UAMINIFU

NI KATIKA SIFA ZA WANAOMPENDA MTUME SAW

Na

Abdulla Talib Abdulla

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetuumba mataifa na makabila mbali mbali ili tujuwane na kushirikiana na akatuletea Mtume ili atuongoze katika kuyakamilisha hayo kwa namna iliyo bora kabisa. Sala na Salaam zimshukie mtukufu wa daraja, Mtume wetu na kigezo chetu, nabii Muhammad S.A.W. pamoja na wafuasi wake wote hadi kitakaposimama kiama. Ama baada ya hayo.

Katika mwezi huu wa Rabiu Awwal waislamu wengi husherehekea kuzaliwa kwa Mtume S.A.W. Ni mnasaba mkubwa kwa Waislamu ambao hujifunza mengi katika tabia za Mtume. Cha kujiuliza; ni kwa kiasi gani tunafaidika kwa kusikia sifa hizi njema za mtume SAW?

Wanasherehekea kwa kumpenda kwao Mtume S.A.W huku wakitambua kuwa kumpenda nabii ni jumla ya kumuamini Allah na ni ukamilifu wa imani kama alivyosema S.A.W ***"Hatokuwa mwenye kuamini mmoja wenu mpaka niwe ni kipenzi zaidi kwake kuliko mtoto wake, mzazi wake na watu wake wote"*** bali hata nafsi yake. Kilichomaarufu ni kuwa Mwenye kupenda huwa mtiifu sana kwa Yule anaempenda. Jee utiifu wetu kwa Mtume SAW tunauweka katika daraja gani na kima gani tukiulinganisha na utiifu wetu kwa wake au waume zetu; mabosi au viongozi wetu; marafiki au wasiri wetu, wafadhili au

wahisani wetu? Nafsi inajijua yenyewe, hebu na ijiulize kwa ukweli kabisa Mtume yupo katika nafasi ya ngapi? Na jee hili linaridhiwa na Allah?

Kumpenda Mtume S.A.W kunapelekea kumtukuza, kumfuata na kumtanguliza kuliko kiumbe mwengine yeyote. Hii ni kwa sababu Allah S.W amesema ***((Enyi mlioamini mtiini Allah na mtiini Mtume))*** {Nisaa:59} na akasema **((*Na mtiini Mtume ili mpate kurehemewa))*** {Nur:56}. Pia akatutahadharisha kumpinga kwa namna yoyote kama alivyosema ***((Na watahadhari wale ambao wanakhalifu amri yake isije ikawafika fitna (mtihani) au adhabu inayoumiza))***.{Nur:63}.

Hebu njooni pamoja nami tuwaangalie masahaba wa Mtume S.A.W namna walivyompenda na kumuweka Mtume. Amesimulia Uruwat bin Masoud katika kisa cha Hudaibia***."Wallah nimekwenda kwa wafalme wengi wakiwemo Kisra (Mfalme wa Waaejemi), Kay-swar (Mfalme wa Warumi) na Najjash (mfalme wa Wahabeshi) lakini wallahi sijaona mtu anaeadhimishwa na kutukuzwa zaidi na wafuasi wake kuliko wafuasi wa Muhammad wanavyomtukuza Muhamad...".*** Huyu ni balozi wa makureishi na anayazungumza haya hali yakuwa hakuna adui mkubwa kwake kuliko mtume na wafuasi wake. Aidha anazungumza akiwa na elimu na uzoefu mkubwa wa ulimwengu uliowazunguka kwani alikuwa ni mwanadiplomasia wa makureishi ambae akiranda huku na kule kuchunga maslahi na siasa za nje za Makureishi na watu wa Makka.

Ndugu wapenzi wa Kiislam, kumpenda Mtume kwa mdomo mtupu bila vitendo hakutokuletea faida bali kunaweza kuwa ni kuidanganya nafsi na kuingia katika kundi la watu waovu wanaosema wasiyoyatenda. Hivyo tumpende kwa moyo na kumfanya kuwa ni kigezo katika vitendo vyetu, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu **((Kwa hakika mna kigezo chema kwa Mjumbe wa**

Allah...))*Ahzaab 21*. Na miongoni mwa sifa ambazo alisifika nazo Mtume SAW hata kabla ya kupewa utume ni sifa ya uaminifu yaani Al-Amana.

Uaminifu ni miongoni mwa sifa njema, na ni taji lenye thamani kubwa ambalo humnyanyua mwanadamu hadi kufika katika vilele vya utukufu. Hakika uaminifu ni daraja isiyomithilika, ni nguvu isiyoshindika na ni hadhi ambayo watu huitamani na shingo zikainyenyekea na kuitumikia. Uaminifu ni wajibu kwa muumin, ni mtaji wa mfanyabiashara, ni siri ya kufaulu kwa mtumishi, ni sababu ya umashuhuri wa fundi, ni msingi wa mapenzi ya ndoa na ni ufunguo wa maendeleo kwa ushirika, jamii, au uma wowote ule.

Makureishi kwa umoja wao walimtunuku Mtume S.A.W sifa ya "Swadikul-Amin" yaani mkweli-mwaminifu. Alikuwa ni kituo cha thika kwa wote, walimuwekea mali zao na wakampelekea haki zao na wakamkabili katika matatizo yao. Nae kwa uaminifu wake alitekeleza kwa mujibu wa matakwa ya mtu. Hakutoa siri za adui zake wala hakumkhini alietaka ushauri wake. wakati alipoamrishwa kuhajiri alimbakisha Makka na kumuweka kaimu mtoto wa Ami yake Ali bin Abu Talib R.A ili arejeshe mali na haki za watu. Hii ni daraja kuu ya uaminifu. Watu wamemkusanyikia wamuue nae bado anawarejeshea amana zao. Hebu tujiangalie vipi kwa upande wetu tunachunga uaminifu katika dini yetu, kazi zetu, ndoa zetu na mambo yetu yote?

Kwa hakika uaminifu ulikuwa ni sifa iliyochomoza katika zama za awali za uislamu. Huyu hapa khalifa wa pili Omar bin Khatwab –Allah amridhie- anapita mitaani alfajiri ili kuangalia hali za raia wake, mara anamsikia mwanamke anamwambia binti yake achanganye maziwa na maji ili wakauze. Binti akamjibu mama yake kuwa wasilifanye hilo na akatoa udhuru kwa vile Sayyidna na Umar amekataza kufanya hivyo. Mama akajibu "Na yuko wapi huyo Umar kwani anatuona". Binti Muaminifu akajibu "Kama Omar hatuoni bila ya shaka Mola wa Omar anatuona". Yalayti kauli hii ingekuwemo katika moyo wa kila

mfanyabiashara, dalali, mwanahabari au alieaminika kwa jambo lolote. Tusingekuwa na bidhaa zilizopita muda au zilizo chini ya kiwango. Tusingekuwa na habari za uongo au uchochezi; na tuzingebebeshana mizigo mikubwa ya kupandishiana bei isivyo na haki.

Wakati waislamu walipofungua miji ya Qaadisiyya baada ya kuwashinda wafursi, Jemedari wa kiislamu Saad bin Abi Waqas alipelekewa dhahabu, fedha na funguo za hazina za Kisra zilizosheheni mirundo ya mali. Alipoona wingi wa mali hizo alitokwa na machozi, akawakusanya masahaba na makamanda wa jeshi. Akawambia "Hii mali ni amana iliyopitishwa mikononi mwenu, je tuifanye nini?". Wakasema kwa sauti moja, kwa moyo mmoja: "Tunaona mali yote uipeleke kwa Kiongozi wa Waislamu Omar bin Khatwab". Hawakuchukuwa asilimia kumi , wala dirhamu wala punje moja ya mali. Waislamu nguo zao zimechakaa, mikuki yao imekatika, familia zao zina matatizo mengi, nao wana uhitaji mkubwa wa mali, wana kiu na njaa ambayo Allah pekee ndie aijuae lakini wakaipeleka mali yote kwa Khalifa Omar ili aitumie kwa kuangalia maslahi ya dola . Basi Omar alipoiona mali ile alilia na akasema "Naapa kwa Allah ambae hakuna Mola ila Yeye hakika watu waliofanya haya ni waaminifu".

Hakika uaminifu ni uwanja mpana na una nyanja nyingi zinazofungamana na haki za Allah, haki za waja na haki za mtu kwa nafsi yake. Haki kubwa kuliko zote ni neno la tawhid *"Laailaha illa llah Muhammadu rasulullah"* Yaani hapana mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki ila mwenyezi Mungu na hakika ya Muhammad ni mjumbe wake . Jee tunalisema na kulitekeleza kivitendo katika ibada zetu, nyumba zetu, kazi zetu na maisha yetu yote au tumeliwekea nyakati chache na sehemu maalumu tu?

Kila mtu anapotamka neno ajue ni amana; anapotoa habari, kisa au riwaya ni amana; anapopiga hatua kuliendea jambo lolote ni amana; anapotoa hukumu

kwa mtu, jambo au tukio ni amana; na yote ni mas-ulia na dhamana kubwa na nzito ambazo zitadumu uhai wote na kuwekewa hesabu yake siku ya kiama.

Elimu ni amana katika shingo za wasomi na wanachuoni. Iwapo watakuwa waaminifu kwa kuisomesha na kuitumia kwa maslahi yao na jamii zao, wakaibainisha na kuitawanya ili kuandaa kizazi kifikra na kivitendo, kidini na kidunia hapo watakuwa ni wakweli na waaminifu wanaostahiki thawabu kutoka kwa Allah na heshima kutoka kwa jamii na watu wao. Ama anaeifanyia ubahili elimu yake, au akaishushia hadhi kwa kutaka umashuhuri au kusifiwa; kipato au cheo; akaifanya shahada au ijaza yake ni hati ya kuonyeshwa au pambo la kutundikwa; au akaleta migawanyiko katika jamii au fitna na mitafaruku, hapo atakuwa hakukusudia kutaka radhi za Allah na bila shaka atakuwa ameikhini amana na hakuwa muaminifu kwa watu wake. Atambue kuwa jasho la wengi limevua na mali za wanajamii wengi zimetumika na ndizo zilizomsogeza hadi akafikia kupata shahada ya Uzamivu au Uzamili, akaitwa mhandisi au daktari bingwa. Jee ni uaminifu kuwafanya watu hawa kuwa watumwa au kutokulipa shukrani. Mtume SAW anasema ***"Atakaekufanyieni wema mlipeni na kama hamna cha kumlipa basi muombeeni dua".*** Msomi wa kweli anapohitajika hunufaisha na asipohitajika hujinufaisha nafsi yake kwa alichokisoma.

Na katika uaminifu ni kutekeleza haki za viongozi, wafanyakazi au watumishi wako, sawa kama hizo ni kubwa au ndogo. Madhali mlikubaliana kuwa utakuwa ni wajibu wako na huendi kinyume na maamrisho ya Allah basi utalazimika kuzitekeleza bila ya kusimamiwa. Tujue kuwa alietawazwa cheo au kupewa dhamana ndogo au kubwa, hakupata ghanima wala mfupa wa kung'ong'ona bali hiyo ni amana na masulia ambayo hesabu yake inamsubiri siku ya kiama . Hivyo, wanaolea mayatima, wasimamizi wa mali za Wakfu, waliopewa wasia, wanaokusanya mapato ya uma, walioajiriwa kutoa huduma ikiwa ni za ujumla au makhsusi vyote hivyo ni amana inayohitaji uaminifu mkubwa na bila shaka

itahesabiwa kwa kila kitu na yule ambae hakifichiki kwake chochote. Anatwambia kipenzi chetu SAW **" *Mche Mwenyezi Mungu popote ulipo".***

Katika uaminifu ni kuhifadhi misingi ambayo dini imeihifadhi na kutilia mkazo ihifadhiwe. Misingi hiyo ni kuhifadhi utukufu wa dini, nafsi, mali na heshima za watu. Kila mmoja ajue kuwa ataulizwa mbele ya Allah kuhusu haya na atahesabiwa ushiriki wake. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu ***((Basi atakaefanya wema hata kama ni wa uzito wa kitu kidogo kabisa ataona jaza yake, na atakaefanya uovu hata kama ni wa uzito wa kitu kidogo kabisa ataona jaza yake*))**. Pia tukumbuke kauli ya Mtume SAW ***"Atakaeona miongoni mwenu uovu, basi na auzuwie kwa mkono wake na asipoweza basi kwa ulimi wake na asipoweza basi na achukie na huo ndio mwisho(udhaifu) wa imani."***

Ndugu waislam, Ili kuthibitisha mapenzi yetu kwa Mtume tujitahidini kuwa waaminifu na kutafuka elimu ya kumjua Mtume ili tujipambe nayo katika maisha yetu yote. Tukifuata nyayo za Mtume wetu tutapata maisha bora hapa Duniani na akhera twendako. Amesema kipenzi chetu Mtume Muhammad SAW: ***"Nimekuachieni jambo ambalo mkishikamana nalo hamtopotea baada yangu wala hamtopata tabu, kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna zangu"***

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mola wa arshi ilio kuu atuwafikishe katika yale anayoyapenda na anayoyaridhia, Mola wetu tupe hekima na utuunganishe pamoja na watu wema, utujaalie tutajwe kwa wema na watakaokuja baada yetu na utujaalie kuwa warithi wa pepo zenye neema, sisi na masheikh zetu na wazee wetu waliotangulia . Wala usitufedheheshe siku ya kufufuliwa .

Wabillahi taufiq, wasalamun alaikum warahmatullah wabarakaatuh.